TANGAZO LA SERIKALI NA. 137 la tarehe 22/5/2026

SHERIA YA BARAZA LA SANAA LA TAIFA,
(SURA YA 204)

# KANUNI

KANUNI ZA BARAZA LA SANAA LA TAIFA ZA MWAKA 2026

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Fasili.

SEHEMU YA PILI
UTENDAJI KAZI WA BARAZA

4. Baraza kufanya kazi kwa kushirikiana na kamati ya wilaya, mikoa na wasajili wasaidizi.
5. Majukumu ya Kamati za wilaya na mikoa.
6. Kamati za Baraza.
7. Kamati ya Maendeleo ya Sanaa Fedha na Mipango.
8. Majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Sanaa, Fedha na Mipango.
9. Kamati ya Rasilimaliwatu na Utawala.
10. Majukumu ya Kamati ya Rasilimaliwatu na Utawala.
11. Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi.
12. Majukumu ya Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi.
13. Kamati ya Sanaa ya Mkoa.
14. Kamati ya Sanaa ya Wilaya.
15. Vikao vya Kamati ya sanaa ya wilaya na mkoa.

SEHEMU YA TATU
USAJILI NA UTOAJI WA VIBALI VYA KAZI ZA SANAA

16. Mamlaka ya Baraza ya usajili na utoaji wa vibali.
17. Wasajili wasaidizi.
18. Takwa la usajili.
19. Wasajiliwa wa Mamlaka nyingine za Serikali.
20. Uzingatiaji wa maadili.
21. Hatua za kuchukua dhidi ya ukikwaji wa maadili.
22. Maamuzi ya Baraza.
23. Maombi ya usajili.
24. Matakwa ya usajili.
25. Kwaya na fani nyingine za sanaa za taasisi za dini na Serikali.
26. Msajili anaweza kukataa maombi ya usajili.
27. Katiba na miongozo mbalimbali.
28. Marekebisho ya taarifa baada ya usajili.
29. Uwasilishaji wa taarifa kwa msajili.
30. Mamlaka ya Msajili kutaka taarifa.
31. Kuvunjika kwa vyama au vikundi vya sanaa.
32. Kufutwa kwa usajili.
33. Taratibu kabla ya kufutiwa usajili au kibali.
34. Usajili wa vyama vya sanaa vya wilaya, mikoa taifa na shirikisho.

SEHEMU YA NNE
MATUKIO YA SANAA

35. Uratibu wa matukio ya sanaa.
36. Kibali cha matukio ya sanaa.

SEHEMU YA TANO
KUMBI ZA SANAA

37. Madaraja ya kumbi.
38. Muda wa matumizi ya kumbi.

SEHEMU YA SITA
MAONESHO YA SANAA NDANI NA NJE YA NCHI

39. Maonesho ya sanaa ndani na nje ya nchi.
40. Wasanii wa kigeni.
41. Uthibitisho wa uwezo wa kumudu gharama.

SEHEMU YA SABA
DAWATI LA SHERIA, MAADILI NA USULUHISHI

42. Muundo na majukumu ya dawati.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI MENGINEYO

43. Ulinzi wa sanaa za jadi.
44. Ulinzi wa mtoto msanii.
45. Adhabu ya jumla.
46. Ukaguzi.
47. Baraza kukuza na kuendeleza sanaa.
48. Rufaa dhidi ya maamuzi ya Baraza.
49. Kufutwa.

---

MAJEDWALI

---

SHERIA YA BARAZA LA SANAA LA TAIFA,
(SURA YA 204)

## KANUNI

(*Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 16)*

KANUNI ZA BARAZA LA SANAA LA TAIFA ZA MWAKA 2026

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za Mwaka 2026.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika kusimamia kazi zote za sanaa Tanzania Bara.

Fasili

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"asasi" maana yake ni taasisi ya Serikali au isiyo ya Serikali iliyosajiliwa na mamlaka husika kwa mujibu wa sheria za nchi na kupewa kibali cha kufanya shughuli za sanaa;

Sura ya 204

"Baraza" maana yake ni Baraza la Sanaa la Taifa lililoanzishwa chini ya Sheria;

"burudani" maana yake ni shughuli zinazofanywa kwa lengo la kufurahisha, kustarehesha, kuelimisha au kuzalisha kipato kwa kutumia kazi ya sanaa;

"chama" maana yake ni muungano wa watu au vikundi zaidi ya kimoja vinavyojishughulisha na fani ya sanaa inayofanana, unaoongozwa na katiba inayotambuliwa na Baraza;

"manjumuziki" maana yake ni mtu anayechagua, kuchanganya au kuchezesha nyimbo za muziki katika matukio ya burudani, eneo la starehe au sherehe;

"kazi za sanaa" ina maana kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"kikundi" maana yake ni muungano wa wasanii zaidi ya mmoja unaoundwa kwa lengo la kufanya kazi za sanaa zinazofanana unaoongozwa na katiba inayotambuliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"kibali" maana yake ni ruhusa ya maandishi inayotolewa na Baraza kwa mtu, kikundi au asasi inayojishughulisha na kazi za sanaa, kwa madhumuni ya kuruhusu utekelezaji wa kazi za sanaa;

"maadili" maana yake misingi, kanuni na mienendo inayokubalika katika jamii ikiwa ni pamoja na kuzingatia tabia njema katika utekelezaji wa kazi za sanaa;

"mdau wa sanaa" maana yake ni mtu, taasisi au kampuni inayoshiriki au inayohusika moja kwa moja au kwa njia nyingine halali, katika masuala ya sekta ya sanaa;

"miundombinu ya sanaa" maana yake ni eneo la wazi, jengo au sehemu nyingine yoyote inayotumika kufanyia kazi za sanaa kwa madhumuni ya burudani, sherehe, urembo, ulimbwende na utanashati;

"msanii" maana yake ni mtu anayejishughulisha au anayefanya kazi za sanaa, binafsi au kwa kushirikiana na wengine kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"mtandao" maana yake ni muungano wa wasanii au wadau wa sanaa bila kujali ufanano wa fani zao unaoongozwa na katiba inayotambuliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Msajili" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Baraza au afisa mwingine aliyeidhinishwa, mwenye mamlaka ya kusajili wasanii na wadau wa sanaa;

"msajili msaidizi" maana yake ni Afisa Utamaduni katika halmashauri husika ambaye amekasimishwa kwa maandishi na Baraza kutekeleza majukumu ya usajili kwa kwa mujibu wa kanuni hizi;

Sura ya 13 "mtoto" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mtoto;

"sanaa" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

"sanaa za jadi" maana yake ni sanaa za kimapokeo zinazorithishwa kizazi hadi kizazi na kuakisi utamaduni, mila, familia, kabila au enzi husika; na

"shirikisho" maana yake ni muungano wa vyama vya sanaa vya fani husika unaoongozwa na katiba

inayotambuliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi au miongozo iliyoandaliwa chini yake.

## SEHEMU YA PILI
## UTENDAJI KAZI WA BARAZA

Ushirikiano wa Baraza na kamati za sanaa za mikoa na za wilaya na wasajili wasaidizi

**4**. Baraza litatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na kamati za sanaa za mikoa na wilaya na ambazo zitafanya kazi kwa niaba ya Baraza katika maeneo yao husika kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Majukumu ya kamati za mikoa na wilaya

**5**. Kamati za mikoa na wilaya zitakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kukuza na kuendeleza kazi za sanaa katika mikoa na wilaya, ikiwemo kuibua na kuhifadhi sanaa za asili kwa kufanya tafiti za sanaa;

(b) kufanya tafiti kuhusu maendeleo, uzalishaji na viwango vya kazi za sanaa katika mikoa na wilaya husika;

(c) kutoa ushauri na msaada wa kiufundi kwa wasanii, vikundi na asasi zinazojishughulisha na kazi za sanaa katika wilaya au mkoa husika;

(d) kuandaa mipango na kuratibu shughuli za sanaa zinazofanywa na watu au asasi mbalimbali katika wilaya au mkoa husika;

(e) kulishauri Baraza kuhusu masuala yanayohusu maendeleo na ukuzaji wa kazi za sanaa katika wilaya, mkoa na Taifa kwa ujumla;

(f) kutoa na kuratibu mafunzo kwa wasanii na wadau wa sanaa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika sekta ya sanaa;

(g) kusaidia na kushauri wasanii au asasi katika masuala yanayohusu uingizaji wa bidhaa za sanaa kutoka nje ya nchi na ukuzaji wa kazi za sanaa nje ya nchi kwa mujibu wa sheria husika;

(h) kuhimiza maendeleo ya kazi za sanaa kwa kuandaa na kuratibu matukio ya sanaa, warsha na semina kwa wasanii na wadau wa sanaa;

(i) kuandaa na kuwasilisha kwa Baraza taarifa za utekelezaji wa majukumu ya kamati kwa kila robo mwaka; na
(j) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa maelekezo ya Baraza au kwa faida ya maendeleo ya sanaa katika wilaya, mkoa na Taifa kwa ujumla.

Kamati za Baraza

**6.**-(1) Baraza linaweza kuunda kamati za kudumu au za muda ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Baraza linaweza kuunda kamati zifuatazo kama kamati za kudumu kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa majukumu yake:
(a) Kamati ya Maendeleo ya Sanaa, Fedha na Mipango;
(b) Kamati ya Rasilimaliwatu na Utawala; na
(c) Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi.

Kamati ya Maendeleo ya Sanaa, Fedha na Mipango

**7**.-(1) Kamati ya Maendeleo ya Sanaa, Fedha na Mipango itakuwa na wajumbe wafuatao:
(a) mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza wenye uelewa wa masuala ya fedha au mipango, ambaye atakuwa Mwenyekiti; na
(b) wajumbe wengine wasiopungua wawili na wasiozidi watatu kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza wenye uelewa na utaalamu katika masuala ya sanaa, fedha au mipango.

(2) Mkurugenzi Msaidizi wa Baraza anayehusika na masuala ya sanaa, utafiti na masoko atakuwa Katibu wa Kamati.

Majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Sanaa, Fedha na Mipango

**8**. Kamati ya Maendeleo ya Sanaa, Fedha na Mipango itakuwa na majukumu yafuatayo:
(a) kuchambua na kubainisha mahitaji ya maendeleo ya sanaa;
(b) kupitia na kulishauri Baraza kuhusu utafiti za sanaa;
(c) kujadili na kupitisha kalenda ya matukio ya sanaa;
(d) kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ya sanaa;

(e) kushauri kuhusu vyanzo na mikakati ya mapato ya Baraza kwa kuzingatia vyanzo vya mapato vilivyoainishwa kwenye Sheria;
(f) kupitia na kupendekeza mpango kazi, bajeti ya mwaka, na mpango mkakati wa Baraza;
(g) kujadili taarifa za mapato na matumizi;
(h) kusimamia utekelezaji wa miongozo ya Serikali na ya kimataifa kuhusu usimamizi wa fedha;
(i) kupendekeza kanuni za fedha za Baraza; na
(j) kutekeleza majukumu mengine kama Baraza litakavyoelekeza.

Kamati ya Rasilimali watu na Utawala

**9**.-(1) Kamati ya Rasilimaliwatu na Utawala itakuwa na wajumbe wafuatao:
(a) mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza, ambaye atakuwa Mwenyekiti; na
(b) wajumbe wengine wasiozidi wawili kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza, ambapo mmoja atapaswa kuwa mwenye utaalamu katika masuala ya rasilimaliwatu.

(2) Mkurugenzi Msaidizi wa Baraza anayehusika na masuala ya rasilimaliwatu atakuwa Katibu wa Kamati.

Majukumu ya Kamati ya Rasilimali watu na Utawala

**10**. Kamati ya Rasilimaliwatu na Utawala itakuwa na majukumu yafuatayo:
(a) kupendekeza muundo wa kiutumishi, mpango wa huduma na ikama ya watumishi;
(b) kupendekeza miongozo ya ndani ya utumishi;
(c) kupitia na kupendekeza mpango wa mafunzo na maendeleo ya watumishi;
(d) kushauri kusimamia masuala ya kinidhamu ya watumishi;
(e) kupitia na kupendekeza kanuni za ndani za utumishi na utawala; na
(f) kutekeleza majukumu mengine kama Baraza litakavyoelekeza.

**11**.-(1) Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi itakuwa na wajumbe wafuatao:

Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi

(a) mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza wenye uelewa wa masuala ya usimamizi wa fedha ambaye atakuwa Mwenyekiti; na
(b) wajumbe wengine wasiopungua wawili kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza.

(2) Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani cha Baraza atakuwa Katibu wa Kamati.

Majukumu ya Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi

**12**. Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi itakuwa na majukumu yafuatayo:
(a) kusaidia Baraza kusimamia utawala bora na udhibiti wa ndani wa fedha na vihatarashi;
(b) kupitia taarifa za ukaguzi wa ndani na nje na kutoa mapendekezo;
(c) kufuatilia usimamizi wa vihatarishi; na
(d) kutekeleza majukumu mengine kama Baraza litakavyoelekeza.

Kamati ya Sanaa ya Mkoa

**13**.-(1) Baraza litaunda Kamati ya Sanaa ya Mkoa kwa kila mkoa itakayokuwa na wajumbe wafuatao:
(a) Katibu Tawala wa Mkoa, ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Afisa Utamaduni wa Mkoa ambaye atakuwa Katibu;
(c) Maafisa Utamaduni wa wilaya zote za mkoa husika; na
(d) wajumbe wengine wasiozidi watatu watakaoteuliwa na Baraza.

(2) Baraza linaweza kuteua mjumbe kujaza nafasi iliyo wazi katika wajumbe waliobainishwa katika kanuni ndogo ya (1) kwa sababu ya kujiuzulu, kuondolewa katika nafasi ya ujumbe, kifo au sababu nyingine.

Kamati ya Sanaa ya Wilaya

**14**. Kutakuwa na Kamati ya Sanaa ya Wilaya itakayojumuisha-
(a) Katibu Tawala wa Wilaya, ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;
(b) Afisa Utamaduni wa Halmashauri, ambaye atakuwa Katibu;

(c) wajumbe wengine wasiozidi watatu watakaoteuliwa na Baraza; na
(d) mweka hazina wa Halmashauri.

Vikao vya kamati ya sanaa ya mikoa au wilaya

**15**. Kamati ya sanaa ya wilaya au mkoa itafanya vikao vya kawaida angalau mara nne kwa mwaka na inaweza kufanya kikao cha dharura pale inapobidi.

## SEHEMU YA TATU
## USAJILI NA UTOAJI WA VIBALI VYA KAZI ZA SANAA

Mamlaka ya Baraza ya usajili na utoaji wa vibali

**16**.-(1) Bila kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, Baraza litakuwa na mamlaka ya-
(a) kusajili wasanii, vikundi, vyama, mitandao, mashirikisho, miundombinu au vituo vinavyojihusisha na kazi za sanaa; na
(b) kutoa vibali kwa watu, taasisi au kampuni zinazojihusisha na kazi za sanaa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), msanii au mdau wa sanaa asiye raia wa Tanzania atasajiliwa au kupewa kibali baada ya kuthibitisha kuwa ana kibali halali cha ukazi nchini kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja kwa madhumuni ya kufanya kazi za sanaa.

(3) Kibali kitakachotolewa chini ya kanuni hii kitakuwa halali kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu kutolewa kwake.

Wasajili wasaidizi

**17**.-(1) Msajili atatekeleza majukumu yake kwa kusaidiwa na wasajili wasaidizi ambao ni Maafisa Utamaduni wa Mikoa na halmashauri husika, walioidhinishwa na Baraza.

(2) Wasajili wasaidizi watakuwa na majukumu yafuatayo:
(a) kusaidia usajili na utoaji wa vibali kwa wasanii na wadau wa sanaa kwenye mikoa na halmashauri husika;
(b) kuhakikisha matukio ya sanaa yanafanyika baada ya vibali kutolewa;
(c) kufuatilia uzingatiaji wa masharti ya usajili na vibali;

(d) kuhimiza uzingatiaji wa maadili kwa wasanii na wadau wengine wanaojihusisha na kazi za sanaa;
(e) kuwasilisha kwa Msajili taarifa za utekelezaji wa shughuli za sanaa kwa mwezi husika; na
(f) kutekeleza majukumu mengine kama Msajili atakavyoelekeza.

(3) Asilimia ishirini na tano ya mapato yatakayotokana na ada ya usajili na kibali cha mwaka italipwa katika Halmashauri husika anakotekeleza shughuli za sanaa msanii au mdau wa sanaa.

(4) Malipo ya ada chini ya kanuni ndogo ya (3) yatafanywa kwa utaratibu utakaowekwa na Baraza.

Takwa la usajili

**18**.-(1) Msanii au mdau wa sanaa hataruhusiwa kufanya kazi za sanaa bila kusajiliwa na kupewa kibali cha Baraza kwa fani husika.

(2) Usajili na utoaji wa kibali vitafanywa baada ya malipo ya ada kwa viwango kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Wasajiliwa wa Mamlaka nyingine za Serikali

**19**.-(1) Mtu, kampuni, taasisi au asasi zilizosajiliwa na mamlaka nyingine za Serikali zitapaswa kupata kibali cha Baraza kabla ya kujishughulisha na kazi za sanaa.

(2) Kibali chini ya kanuni hii kitahuishwa kila mwaka.

(3) Mtu, kampuni, taasisi au asasi itakayoendelea na shughuli za sanaa bila kuhuisha kibali itakuwa imetenda kosa.

(4) Asasi isiyo ya kiserikali itawasilisha kwa Baraza taarifa za utekelezaji wa shughuli za sanaa kwa mwaka husika.

(5) Endapo kampuni au asasi isiyo ya kiserikali itaacha kufanya shughuli za sanaa itapaswa kutoa taarifa kwa Baraza.

Uzingatiaji wa maadili

**20**.-(1) Msanii au mdau wa sanaa atahakikisha kuwa kazi za sanaa zitakazowasilishwa kwa umma zinazingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya maadili katika kazi za sanaa iliyotolewa na Baraza.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, kazi ya sanaa itakuwa imezingatia maadili endapo itakuwa na sifa zifuatazo:
(a) haivunji heshima ya mwimbaji, msikilizaji au mtazamaji;
(b) haina upotoshaji wa aina yoyote;

(c) haichochei ghasia, fujo, vurugu au uvunjifu wa amani wa aina yoyote;
(d) haina maneno ya uongo, uchochezi au yanayokashifu watu wengine au mamlaka;
(e) haijatumia lugha chafu au matusi;
(f) haina ujumbe wa unyanyasaji au ukatili;
(g) haioneshi ubaguzi wa rangi, kabila au dini;
(h) haikashifu Taifa la Tanzania au mataifa mengine;
(i) haidhoofishi umoja, ushirikiano na ustawi bora wa jamii;
(j) haishawishi wala kuhamasisha vitendo vya ngono, ushoga, usagaji, ulawiti, unajisi wa watoto au matumizi ya dawa za kulevya;
(k) inalenga kuelimisha, kukosoa, kuonya na kuelekeza jamii katika masuala mbalimbali ya ustawi na maendeleo; na
(l) inazingatia masharti ya Sheria za Tanzania katika masuala ya hakimiliki na masuala mengineyo.

(3) Baraza litaweza kukagua kazi yoyote ya sanaa katika hatua yoyote ya utayarishaji, uzalishaji au usambazaji kwa madhumuni ya kuhakikisha uzingatiaji wa maadili.

(4) Kutakuwa na madaraja ya matumizi ya kazi za sanaa kulingana na hadhira na matumizi yake kama ilivyoanishwa katika Jedwali la Tatu .

Hatua za kuchukua dhidi ya ukiukwaji wa maadili

**21**.-(1) Endapo kazi ya sanaa itabainika kuwa ina maudhui yanayokiuka maadili, Baraza litatoa notisi ya maandishi ya kusudio la kuchukua hatua stahiki na kumtaka mhusika afike mbele ya Baraza kwa ajili ya kutoa maelezo.

(2) Mhusika wa kazi ya sanaa iliyobainika kuwa na maudhui yanayokiuka maadili atapewa fursa ya kuwasilisha utetezi wake ndani ya siku saba tangu kutolewa kwa notisi ya maandishi ya kusudio la kumchukulia hatua.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (2), mhusika wa kazi ya sanaa anaweza kuwasilisha utetezi wake yeye binafsi au kupitia mwakilishi.

(4) Endapo Baraza halitaridhika na utetezi uliowasilishwa na mhusika, linaweza kutoa uamuzi kwa kuzingatia taarifa zilizopo.

Uamuzi wa Baraza

**22**.-(1) Baada ya kuzingatia maelezo ya mhusika wa kazi ya sanaa au mwakilishi wake na kujiridhisha kuwa mhusika ana hatia, Baraza linaweza kutoa adhabu moja au zaidi kati ya zifuatazo:

(a) kutoa onyo kali la kutorudia kutenda kosa;
(b) kuisimamisha au kuiondoa kazi ya sanaa katika matumizi;
(c) kumsimamisha au kumfungia mhusika kujishughulisha na kazi za sanaa kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja; au
(d) kutoza faini.

(2) Katika kuamua adhabu chini ya kanuni hii, Baraza litazingatia uzito wa kosa, athari zake kwa jamii na iwapo kosa limerudiwa.

(3) Katika kusimamia utekelezaji wa kanuni hii, Baraza litaandaa mwongozo wa maadili utakaotumiwa na wasanii na wadau wa sanaa katika kuandaa kazi za sanaa.

Maombi ya usajili

**23**.-(1) Maombi ya usajili na utoaji wa vibali utafanywa kwa kutumia mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa taarifa za wasanii na wadau wa sanaa kwa kujaza fomu iliyoanishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya usajili na vibali yataambatana na malipo ya ada kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Matakwa ya usajili

**24**.-(1) Maombi ya usajili au vibali yataambatishwa na-

(a) kwa msanii binafsi au mdau wa sanaa-
  (i) namba ya utambulisho wa uraia;
  (ii) namba ya utambulisho wa mlipa kodi; na
  (iii) taarifa nyingine yoyote ambayo Baraza litaweza kuhitaji;
(b) kwa shirikisho, chama, mtandao, asasi, kituo cha sanaa au kikundi-
  (i) namba ya utambulisho wa uraia wa mmoja wa viongozi;
  (ii) namba ya utambulisho wa mlipa kodi ya taasisi husika;
  (iii) namba ya usajili ya taasisi husika;

(iv) katiba na mpango wa kazi ya sanaa; na
(v) picha za viongozi;

(c) kwa kampuni, namba ya usajili wa kampuni na katiba ya kampuni; na

(d) kwa raia wa kigeni-
(i) hati ya kusafiria;
(ii) kibali halali cha ukazi; na
(iii) taarifa nyingine yoyote ambayo Baraza linaweza kuhitaji.

(2) Baraza baada ya kupokea maombi na kujiridhisha kuwa taarifa zilizowasilishwa na mwombaji ni sahihi na zinakidhi matakwa ya usajili, litatoa cheti cha usajili au kibali ndani ya siku saba tangu tarehe ya kuwasilishwa kwa maombi.

Kwaya na fani nyingine za sanaa za taasisi za dini na Serikali

**25**. Kwaya na fani nyingine za sanaa za taasisi za dini na Serikali zitawasilisha, wakati wa usajili, uthibitisho wa maandishi kutoka kwa uongozi wa taasisi husika.

Msajili anaweza kukataa maombi ya usajili

**26**. Msajili anaweza kukataa maombi ya usajili wa mtu, kikundi, kampuni au asasi iwapo-

(a) jina linalopendekezwa kusajiliwa linafanana na jina ambalo tayari limeshasajiliwa;
(b) shughuli za sanaa zinazopendekezwa zinakiuka sheria za nchi;
(c) malengo ya shughuli ya sanaa yanaweza kuhatarisha usalama au amani ya jamii;
(d) maombi husika ya usajili yanapaswa kufanywa chini ya mamlaka nyingine.

Masuala yatakayobainishwa katika Katiba

**27**. Katiba ya mwombaji inayowasilishwa wakati wa usajili itabainisha-

(a) jina na anwani kamili;
(b) uanachama na masharti yake;
(c) madhumuni na shughuli inayofanywa;
(d) muundo na utaratibu wa uendeshaji;
(e) uhusiano na Baraza;
(f) mgawanyo wa mali na madeni endapo taasisi itavunjika;

(g) vyanzo vya mapato na uwazi wa mikataba;
(h) usawa wa kijinsia na ujumuishaji wa watu wenye ulemavu;
(i) mpango wa usuluhishi wa migogoro;
(j) mpango wa uzingatiaji wa maadili na ulinzi wa mtoto; na
(k) uzingatiaji wa sheria za nchi.

Marekebisho ya taarifa baada ya usajili

**28**.-(1) Pale ambapo mtu aliyesajiliwa atataka kurekebisha taarifa zake za usajili, atawasilisha maombi kupitia mfumo kwa Msajili.

(2) Marekebisho hayataanza kutumika hadi Msajili atakapoyaidhinisha.

Uwasilishaji wa taarifa kwa Msajili

**29**.-(1) Kila msajiliwa au mdau wa sanaa, isipokuwa msanii binafsi au kikundi, atawasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi zake mara mbili kwa mwaka, mwezi Juni na Desemba.

(2) Msajili anaweza kukataa maombi ya kuhuisha kibali ikiwa msajiliwa au mdau wa sanaa atashindwa kuwasilisha taarifa kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1).

Mamlaka ya Msajili kutaka taarifa

**30**.-(1) Msajili anaweza kumtaka msanii au mdau wa sanaa aliyesajiliwa kuwasilisha taarifa yoyote inayohusiana na kazi yake ya sanaa ndani ya muda atakaoubainisha.

(2) Msajili anaweza kufanya ziara za ushauri na ufuatiliaji kwa wasanii na wadau wa sanaa kadri atakavyoona inafaa.

Kuvunjika kwa vyama au vikundi vya sanaa

**31**.-(1) Msanii au mdau wa sanaa anayekusudia kuacha kufanya kazi ya sanaa kwa sababu yoyote, atapaswa kuwasilisha taarifa ya maandishi kwa Msajili kwa kujaza fomu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Msajili atatoa maelekezo stahiki baada ya kupokea taarifa.

Kufuta usajili

**32**. Msajili anaweza kufuta usajili au kibali iwapo msajiliwa au mwenye kibali-

(a) anatumika kuchochea uhasama miongoni mwa jamii kwa kutumia sanaa kwa kujenga tofauti za kisiasa au kidini au ubaguzi wa aina yoyote ile;

(b) anatekeleza shughuli tofauti na ile aliyoidhinishwa kufanya;

(c) anakiuka sheria au kanuni na taratibu zinazoongoza kazi za sanaa; au

(d) anatoa taarifa ya kusudio la kuacha kufanya shughuli za sanaa.

Taratibu kabla ya kufutiwa usajili au kibali

**33**.-(1) Kabla ya kufuta usajili au kibali chini ya kanuni ya 32, Msajili atatoa notisi ya kusudio la kufuta usajili au kibali na kumpa msajiliwa au mmiliki wa kibali fursa ya kujitetea kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), msajiliwa au mmiliki wa kibali anaweza kuwasilisha utetezi wake yeye binafsi au kupitia mwakilishi.

(3) Endapo msajiliwa au mmiliki wa kibali hatatoa utetezi ndani ya siku zilizoainishwa bila sababu ya msingi, Baraza litafuta usajili wake au kibali.

Usajili wa vyama vya sanaa vya wilaya, mikoa taifa na shirikisho

**34**.-(1) Usajili wa vyama vya sanaa utafanyika kwa kuzingatia ngazi zifuatazo:

(a) chama cha sanaa cha wilaya kitaanzishwa na wanachama au vikundi vya fani husika ndani ya wilaya;

(b) chama cha sanaa cha mkoa kitaanzishwa na vyama vya wilaya ndani ya mkoa husika;

(c) chama cha kitaifa kitanzishwa na vyama vya mikoa ya Tanzania Bara; na

(d) shirikisho litaundwa na vyama vya kitaifa vya fani husika.

(2) Chama au shirikisho litakuwa na muundo uliobanishwa katika katiba yake na uliokubaliwa na wanachama wote.

## SEHEMU YA NNE
## MATUKIO YA SANAA

Uratibu wa matukio ya sanaa

**35**.-(1) Baraza litakuwa mratibu wa matukio ya sanaa nchini.

(2) Tukio la sanaa halitafanyika bila kibali cha Baraza.

(3) Asilimia ishirini na tano ya ada ya kibali kwa tukio la sanaa itapelekwa kwenye Halmashauri husika na asilimia sabini na tano ya ada itabaki Baraza.

Kibali cha kufanya tukio la sanaa

**36**.-(1) Kibali cha kufanya tukio la sanaa kitatolewa iwapo-

(a) mwombaji wa tukio amewasilisha kwa Msajili maombi na andiko la mchanganuo wa tukio angalau siku thelathini kabla ya tukio;
(b) tukio limeidhinishwa na Baraza;
(c) ametoa uthibitisho kuwa wasanii wanaoshiriki wamesajiliwa na wana vibali hai;
(d) amewasilisha uthibitisho kuwa kumbi zinazotumika kwa tukio hilo zimesajiliwa na zimepewa vibali hai; na
(e) mwombaji ametoa hakikisho kuwa tukio litaendeshwa kwa kuzingatia maadili na usalama kwa mujibu wa miongozo ya maadili katika kazi za sanaa.

(2) Mwombaji atapewa kibali baada ya maombi yake kupitiwa na kuridhiwa na Baraza na endapo mwombaji atakuwa anafanya tukio lisilo la kibiashara kwa mara ya kwanza atapewa kibali bila malipo na atasimamiwa na Baraza.

(3) Baraza linaweza kukataa maombi ambayo hayajakidhi vigezo kama vilivyoanishwa katika mwongozo unaosimamia uandaaji na uendeshaji wa matukio ya sanaa.

(4) Mwombaji wa tukio baada ya kupewa kibali atapaswa kuhakikisha kuwa tukio linaendeshwa kwa kuzingatia maadili kwa mujibu wa mwongozo unaosimamia uzingatiaji wa maadili katika kazi za sanaa.

(5) Baada ya kupata kibali cha kufanya tukio, mwombaji wa tukio la sanaa atatakiwa kuzingatia ubora wa kumbi zinazotumika kwa ajili ya tukio la sanaa na ikiwa tukio linalohusisha watoto atahakikisha kuwa kumbi ni salama na rafiki kwa matumizi ya watoto ikiwemo wenye ulemavu na kuwa zina ulinzi imara wakati wote wa tukio la sanaa.

(6) Mwombaji aliyepewa kibali cha kufanya tukio la sanaa atapaswa kuwasilisha taarifa ya tukio hilo ndani ya siku thelathini baada ya tukio kufanyika.

(7) Mtu atakayekiuka kanuni hii anatenda kosa na atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu na

isiyozidi shilingi milioni tano au kufungiwa kujihusisha na kazi za sanaa kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

## SEHEMU YA TANO
## KUMBI ZA SANAA

Madaraja ya kumbi

**37**.-(1) Baraza litasajili kumbi za sanaa kwa madaraja kulingana na miundombinu, usalama na matumizi kama ifuatavyo:

(a) Daraja A litajumuisha kumbi zenye sifa zifuatazo:
  (i) miundombinu ambayo hairuhusu sauti na mitetemo kutoka nje;
  (ii) vifaa vya kuingiza hewa ndani;
  (iii) milango inayofunguka kwa nje;
  (iv) vifaa vya kuzimia moto;
  (v) vyoo nadhifu kwa jinsia zote;
  (vi) maegesho;
  (vii) miundombinu ya kuwawezesha watu wenye ulemavu;
  (viii) vifaa vya ulinzi na usalama;
  (ix) milango ya dharura;
  (x) alama za kutoka nje; na
  (xi) eneo maalumu kwa ajili ya kuvutia sigara;

(b) Daraja B litajumuisha kumbi au maeneo ya wazi ambayo miundombinu yake ina sifa zifuatazo:
  (i) inawezesha watu wenye ulemavu kutumia kwa urahisi;
  (ii) ina vifaa vya kuingiza hewa ndani;
  (iii) ina milango na madirisha yanayofunguka kwa nje;
  (iv) ina vifaa vya kuzimia moto;
  (v) ina vyoo nadhifu kwa jinsia zote;
  (vi) ina maegesho; na
  (vii) ina vifaa vya ulinzi na usalama; na

(c) Daraja C litajumuisha kumbi au maeneo ya wazi ambayo yapo katika sehemu au eneo ambalo kuna huduma zote muhimu za kijamii japo hazipo katika viwango vya Daraja A na B.

Muda wa matumizi ya kumbi

**38**.-(1) Kumbi zitatumika kwa ajili ya maonesho ya kazi za sanaa, burudani na sherehe kwa utaratibu ufuatao:

(a) kumbi za Daraja A zinaweza kutumika muda wote;

(b) kumbi za Daraja B zinaweza kutumiwa kuanzia saa kumi jioni hadi saa sita usiku kwa siku za Jumatatu hadi Ijumaa:

Isipokuwa kwamba, kwa siku za Jumamosi, Jumapili au siku za sikukuu zitatumika kuanzia saa sita mchana hadi saa nane usiku; na

(c) kumbi za Daraja C zinaweza kutumiwa kuanzia saa kumi jioni hadi saa nne usiku.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Baraza linaweza kuongeza muda wa maonesho kwa ukumbi husika baada ya kupokea maombi kutoka kwa mwombaji.

(3) Mmiliki yeyote wa ukumbi atakayekiuka masharti ya kanuni hii anatenda kosa.

## SEHEMU YA SITA
## MAONESHO YA SANAA NDANI NA NJE YA NCHI

Maonesho ya sanaa ndani na nje ya nchi

**39**.-(1) Msanii, kikundi au mdau wa sanaa anaweza kufanya maonesho ya sanaa nje ya nchi baada ya kupata kibali cha Baraza.

(2) Maombi ya kibali yataambatishwa na nyaraka zifuatazo:

(a) barua ya maombi ya kibali cha safari;

(b) barua ya mwaliko au nakala ya mkataba wa kazi za sanaa uliosainiwa na msanii pamoja na waandaaji wa tukio husika;

(c) nakala ya hati ya kusafiria ya msanii; na

(d) nyaraka nyingine kama Baraza litakavyoona inafaa.

(3) Baada ya kupokea maombi na kujiridhisha kuwa mwombaji anastahili kupata kibali, Baraza litatoa kibali.

(4) Msanii, kikundi au mdau wa sanaa aliyepewa kibali chini ya kanuni hii, atapaswa kuwasilisha taarifa kuhusu maonesho aliyoyafanya ndani ya siku ishirini na moja baada ya maonesho hayo.

(5) Msanii, kikundi au mdau wa sanaa anayekiuka masharti ya kanuni hii anatenda kosa na atalipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi milioni tatu.

Wasanii wa kigeni

**40**. Msanii, kikundi au mdau wa sanaa kutoka nje ya nchi anayeingia nchini kwa ajili ya kufanya kazi ya sanaa kibiashara, ataombewa kibali kwa Baraza na maombi hayo yataambatana na malipo ya ada kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili:

Isipokuwa kwamba, maombi ya kibali kwa msanii, kikundi au mdau wa sanaa anayeingia nchini kwa lengo la kuwajengea wasanii au vikundi vya ndani ya nchi au wadau wa sanaa uwezo, au kwa lengo la kujenga mahusiano ya kidiplomasia, hayataambatana na malipo ya ada.

Uthibitisho wa uwezo wa kumudu gharama

**41**. Msanii anayetaka kwenda nje ya nchi au msanii wa kigeni anayetaka kuingia nchini kwa ajili ya kufanya maonesho nchini, atapewa kibali baada ya mwombaji kuthibitisha uwezo wake wa kumudu gharama za uendeshaji wa maonesho hayo na gharama za mwombaji kujikimu akiwa ugenini au hapa nchini.

## SEHEMU YA SABA
## DAWATI LA SHERIA, MAADILI NA USULUHISHI

Muundo na majukumu ya dawati

**42**.-(1) Kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi na utekelezaji bora wa masharti ya kanuni hii, Baraza litaanzisha dawati la sheria, maadili na usuluhishi.

(2) Dawati litakaloanzishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) litakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kusikiliza na kuchambua masuala yanayohusu sheria na maadili na kushauri namna bora ya usuluhishi;

(b) kusikiliza na kusuluhisha migogoro na malalamiko miongoni mwa wasanii na wadau wa sanaa; na

(c) kutekeleza jukumu lolote linalohusiana na majukumu yake kadiri itakavyoelekezwa na Baraza kwa maslahi ya kuendeleza sekta ya sanaa.

(3) Dawati litawasilisha kwa Baraza taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kila robo ya mwaka au kwa kipindi kingine chochote kadiri itakavyoelekezwa.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Ulinzi wa sanaa za jadi

**43**. Mtu hataruhusiwa kutumia au kutengeneza sanaa za jadi kwa madhumuni ya kibiashara nje ya muktadha wa jamii husika bila kupata kibali kutoka kwa Baraza:

Isipokuwa kwamba, kibali hicho hakitahitajika endapo matumizi ya sanaa za jadi yatakuwa ni kwa madhumuni ya kutoa elimu kwa umma pekee.

Ulinzi wa mtoto msanii

**44**.-(1) Mtoto anayejishughulisha na kazi za sanaa atasajiliwa na Baraza na atakuwa chini ya usimamizi wa mzazi au mlezi wake.

(2) Mtu, kikundi, taasisi, kampuni au mdau wa sanaa anayekusudia kumtumia mtoto katika shughuli maalumu ya sanaa atawasilisha maombi ya kibali kwa Baraza cha kumtumia mtoto katika kazi ya sanaa.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2), maombi ya kibali yataambatishwa na vitu vifuatavyo:

